



LIGHT EXAMINATIONS BUREAU(LEB)

“The Academic Epitome”

SENIOR TWO END OF YEAR HOLIDAY PACKAGE 2024

LUGHA YA KISWAHILI

Student’s Name.....Stream.....

LIN No.....Expected Score.....%

INSTRUCTIONS

Attempt all items.

SEHEMU A(INSHA)

ITEM ONE

Hongera! Umeshinda tiketi ya bure kuenda sehemu unayoitaka. Utaenda wapi na kwa nini?

SEHEMU B (UFAHAMU)

ITEM TWO

Soma Habari hii kisha ujibu maswali yatakayofuata.

Ponografia ni tendo, maandishi, picha au michoro inaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, tovuti na kanda za kunasia picha na sauti.

Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea kote ulimwenguni mithili ya moto mbugani wakati wa kiangazi. Kuenea kwake kumechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi ukiwa umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Hata hivyo, kazi hii hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbalimbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la kuvuruga madili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu. Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Kwa mfano, baadhi ya wanamuziki hutumia **ponografia** kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji wa ponografia kuna athari kubwa kwa jamii hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushahidi kuonyesha kuwa wale wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kwamba kinachoonekana kwa jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kisasi ikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama vile masomo, watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera, huyaiga wanayoyaona na kuyasikia. Hii ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Hivyo basi wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa huku wengine wakiambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo yanaweza kuwaletea mauti.

Yasemekana kuwa akili za binadamu hunasa zaidi mambo yanayowalishwa kwa picha na hivyo basi matusi haya yaweza kudumishwa katika kumbukumbu zao. Tabia mbaya kama vie ushoga, ubasha na usagaji huwa matokeo yake na hata matokeo ya vijana hugeuka wanapoanza kuiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, lugha, ishara na miondoko inayohusiana nanngono huibuka. Yote haya yanakinzana na desturi za mwafrica. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kuchapo. Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama vile unywaji pombe na matumizi ya vileo ambavyo huchochea uchu wa ngono na kuibua tabia za kinyama.

Kuendelea kuzitazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, huondoa makali kiasi kwamba hata katika uzima mtu hupoteza mhemko na kugeuswa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mjini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na malezi haya yasiyo na kizuizi.

Kuuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi, watu wazima kuwajibika kwa kuwalinda na kuwahimiza vijana kuhusu maovu haya na wale wenye midahilishi, video na sinema kutowaruhusu

vijana kutazama uchafu huu kunaweza kuwa maana ya kuyakinga au hata kuyaepuka madhara ya ponografia. Ni sharti pia sheria izuie na kupiga marufuku utengenezaji na uenezaji wa upungufu huu. Bila shaka, sheria na hatua kali za ziweze kuchukulia dhidi ya waivunjao. Hali kadhalika, wazazi wasijipweteke tu bali wawaelekeze watoto wao ipasavyo na ila mtu alitekeleze jukumu lake.

Maswali

- (a) Toa sababu za kusambaa kwa uchafu unazozungumziwa katika taarifa.
- (b) **'Bendera hufuata upepo'**. Thibitisha ukweli wa usemi huu kulingana na makala.
- (c) Ni kwa nini ni muhimu kuwakanya vijana dhidi ya uchafu huu?
- (d) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya aina ya uozo unaozungumziwa na mwandishi?
- (e) Fafanua msamiati huu kimuktadha
- (i) **uchu**
 - (ii) **wasijipweteke**
 - (iii) **nishai**

MWISHO

(Tel:+256707270906)

MERRY CHRISTMAS AND A HAPPY NEW YEAR 2025